

A KUTOKA SHERIA HADI NEEMA. Warumi 7:1-6.

- ❖ Mume wa kwanza: Mume ni“sheria” (Yule mzee aliye jaribu kuokolewa kwa kutii sheria). Ikiwa tu tumefunga ndoa na sheria, basi tunafungwa na matakwa yake.
- ❖ Kifo cha Mume wa kwanza: Tunaposulubishwa pamoja na Kristo, utu wa kale unakufa na tunakuwa huru dhidi ya hukumu na mamlaka ya dhambi na sheria.
- ❖ Ndoa mpya: Tunazaliwa katika Roho Mtakatifu tunapoungana katika ufufuo wa Mwokozi; ndipo, tunakuwa hatumtumikii Mungu kwa sheria na hofu tena, bali kwa kuwa tuna roho mpya yenye uhuru na upendo.
- ❖ Tokeo la mwisho ni kubeba matunda ya Mungu; tunda la maisha yaliyorekebishwa.

B UZOEFU WA PAULO. Warumi 7:7-11.

- ❖ Sheria sio dhambi. Dhambi iko ndani ya mwanadamu, na sheria huifunua.
- ❖ Paulo alikuwa Farisayo, aliishi kwa kufuata matakwa ya kikundi chenye sheria kali zaidi katika dini yake. Kwa utunzaji wa sheria wa nje, alikazana bila kuchoka kushika matakwa ya sheria takatifu iliyokuwa ikichunguza moyo.
- ❖ Paulo alipoelewa asili ya kiroho ya sheria, maarifa haya mapya yalimshitaki kwa kuasi na kuzalisha tamaa ya uovu (fungu la 8).
- ❖ Pia aligundua kuwa sheria haituokoi bali inatuhukumu, hivyo akafa. Akaelewa kuwa mwisho wa wadhambi ni kifo cha milele (fungu la 11).

C YA KIROHO NA YA MWILI. Warumi 7:12-14.

- ❖ Ya kiroho: Sheria ya Mungu ni ufunuo wa tabia ya mwandishi wake na maelezo ya mawazo na mapenzi yake. Ilitolewa kwa faida yetu, na ni takatifu yenye haki na njema.
- ❖ Ya kimwili: Dhambi. Tunajikabidhi kwa dhambi tunapoishi tukifuata matakwa ya miili yetu. Hata mwanadamu aliye mtakatifu sana anayo asili ya dhambi akilinganisha na utakatifu wa sheria.
- ❖ Kusudi la kudumu la sheria ni kufunua haki, kufunua dhambi na kuonyesha hitaji la Mwokozi. Kama pasingalikuwapo sheria ya kutuonyesha dhambi, injili isingekuwa na nguvu; kama mdhambi hawezi kuonyeshwa dhambi zake, Hataona hitaji la kutubu na kuwa na imani katika Kristo.

D PAMBANO LA NDANI. Warumi 7:16-20.

- ❖ Je; Nini tunaweza kufanya?
- ❖ “hapa kuna kazi ya mwanadamu kufanya. Lazima akitazame kioo, Sheria ya Mungu, ili kupambanua udhaifu katika tabia yake, na kuziacha dhambi zake, na kuosha vazi lake la tabia katika damu ya mwana kondoo.” E.G.W. (God’s amazing grace, August 11).

E SHERIA MBILI NDANI YA MWANADAMU. Warumi 7:21-25.

- ❖ SHERIA AKILINI
 - Ni kujua mapenzi ya Munqu, yaliyofunuliwa kwa mwanadamu.
 - Nisheria ya Munqu, aliyokubaliwa na akili mwanadamu.
 - Huniongoza kwa Yesu Kristo, anayeniweka huru dhidi ya dhambi.
- ❖ SHERIA NDANI YA WASHIRIKA WANGU
 - Ni nguvu ya uovu inayotengeza matatizo maishani mwanqu
 - Hutumia matamano yanqu ya mwili
 - Hunifanya kuwa mtumwa wa dhambi
- ❖ Tunaweza kuufikia ushindi kupitia kwa YESU KRISTO pekee.